**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**684** **VITENDO VYA KUJIFUNZA SANAA**

**Muda: Saa 3.** **Year: 2013**

---

**Maelekezo.**

1. Karatasi hii ina sehemu **A**, **B** na **C.**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu **A** na maswali **mawili (2)** kutoka katika kila sehemu **B** na **C.**
3. Andika majibu yako kwa kalamu ya wino wa bluu au mweusi isipokuwa michoro ambayo itachorwa kwa penseli.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

**SEHEMU A (Alama 40)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

1. Ainisha sifa nne za zana za kufundishia na kujifunzia somo la Vitendo vya Sanaa.

2. Taja vifaa viwili unavyoweza kuvitumia kuwasilisha dhana ya rangi kwa watoto wa Elimu ya Awali na kwa kila kimoja elezea jinsi utakavyokitumia.

3. Kwa kutumia hoja mbili, tofautisha kati ya mbinu shirikishi na mbinu shirikishi kiasi.

4. (a) Eleza maana ya neno Ufinyanzi.

   (b) Orodhesha misingi miwili ya Ufinyanzi.

6. Ainisha mbinu nne zinazotumika katika kuwafundisha watoto wa Elimu ya Awali mada ya usimulizi wa hadithi.

6. (a) Eleza maana ya wimbo.

   (b) Bainisha hatua tatu za kufundisha wimbo mpya kwa watoto wa Elimu ya Awali.

7. (a) Eleza maana ya neno kupiga chapa.

   (b) Taja vifaa vinne vinavyotumika katika kuchapa maumbo kwa kusugua.

8. Chambua vifaa sita vya uchoraji vinavyotumiwa na watoto wa Elimu ya Awali na kila kimoja eleza sifa yake.

9. Bainisha mbinu nne zinazofaa kufundishia mada ya ufinyanzi kwa watoto wa Elimu ya Awali.

10. Kwa kifupi, eleza maana ya dhana zifuatazo kama zinavyotumika katika ufundishaji na ujifunzaji wa watoto wa Elimu ya Awali:

    (a) Njia

    (c) Zana

    (b) Mbinu

    (d) Makunzi


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU B (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii

11. "Vitendo vya Kujifunza Sanaa ni somo la vitendo zaidi kuliko nadharia." Thibitisha kauli hii kwa kutoa hoja sita.

12. Fafanua mambo sita ya kuzingatia ili muigizaji aweze kufanikiwa katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira.

13. Kwa kutumia hoja tano, onesha umuhimu uliopo kwa watoto wa Elimu ya Awali kujifunza dhana ya uundaji.

## SEHEMU C (Alama 30)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka katika sehemu hii.

14. Fafanua faida sita za tathmini tamati katika somo la Vitendo vya Kujifunza Sanaa.

15. Eleza changamoto tano za ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Vitendo vya Kujifunza Sanaa katika shule za Elimu ya Awali.

16. Kwanini ni muhimu kwa mwalimu kufanya maandalizi kabla ya ufundishaji na ujifunzaji wa dhana ya kuchapa maumbo? Toa sababu tano.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org